# Askofu awapa neno wahadhiri vyuo vikuu

**Na Tumaini Mafie, ARUSHA**

WAHADHIRI wa vyuo vikuu nchini wametakiwa kuwasaidia wahitimu namna bora ya kufaidika na elimu wanayoipata, badala ya kutegemea kuajiriwa.

Rai hiyo ilitolewa na Askofu Mkuu Katoliki Jimbo la Mbulu, Anthony Ragwe, wakati wa mahafali ya Chuo cha Mtakatifu Stephano (SAUT), kusema wahadhiri wanawajibu wa kuhakikisha vijana wanaohitimu wamejengewa uwezo wa kutumia fursa zinazopatikana katika jamii, ili waweze kutoa taswira nzuri kwa jamii na taifa.

"Wasaidieni vijana namna nzuri ya kutengeneza fursa kwa kutumia ubunifu, elimu walioipata pamoja na kuonyesha jamii mabadiliko chanya, kwa hali ilivyo sasa wahitimu wa elimu ya juu ni wengi mtaani ambao hawana ajira, ni vema mkatumia zaidi fursa za kujiajiri kuliko kusubiri ajira," alisema Askofu Rangwe.

Aliongeza kuwa vyuo vinazalisha kwa wingi kuliko mahitaji ya ajira nchini, lakini waangalie namna ya kusaidia ufunguaji wa biashara, namna bora ya kupata mikopo ya riba nafuu, pamoja na kuwasaidia kufungua kampuni binafsi ili waepuke utegemezi.

Aidha, Askofu Ragwe alisema Kanisa Katoliki linaendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha taifa linakuwa na weledi katika fani mbalimbali, kwamba wanatoa elimu kuanzia shule za awali hadi ngazi za juu.

Naye Mkurugenzi wa chuo hicho tawi la Arusha, Padri Charles Rufyiriza, alisema chuo hicho kimewasaidia wanafunzi wengi waliohitimu katika kufungua kampuni binafsi ya utalii mkoani Arusha, kwamba hivi karibuni wanatarajia kuanza kuendesha shughuli za kitalii.

Alisema: "Tuna wanafunzi waliomaliza hapa wameweza kufungua na kusimamia biashara zao, yupo mmoja alimaliza masomo yake ngazi ya stashada na sasa wanamtaji wa Sh. milioni 20, chuo ndiyo tuliomsaidia."



Kaimu Meneja wa Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Mkoa wa Tanga, Dk. Zabron Nziku, akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusu namna walivyofanikiwa kufanya utafiti wa mbegu bora za wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, kuku na vyakula vyao. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Wananchi waikumbusha serikali ujenzi zahanati

**Na Dege Masoli, KILINDI**

WANANCHI wa Kijiji cha Masagalu kilichopo Kata ya Masagalu Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga wameikumbushia serikali kutekeleza ahadi yake ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi hao walidai kuwa kukosekana kwa huduma hiyo ni chanzo cha vifo visivyotarajiwa, vikiwamo vya kinamama na watoto.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Elizabeth Mjema, alisema kinamama wajawazito na watoto wamekuwa wakifariki kutokana na kukosa huduma kwa wakati, kwa sasa wanatembea umbali wa kilometa 28 kufuata huduma ya afya kituo cha Songe.

Mjema alisema hali hiyo ni hatari kwa mama mjamzito kwani licha ya umbali lakini pia ubovu wa miundombinu inamfanya kutumia muda mwingi njiani.

Naye Mwajuma Salehe, alieleza changamoto ya gharama za usafiri kutoka kijijini hapo hadi kituo cha afya cha Songe kwamba ni Sh. 10,000 kwa usafiri wa pikipiki, Sh. 50,000 kwa gari.

Diwani wa Kata hiyo, Munga Mndaila alisema wananchi hao waliamua kuanza ujenzi huo kama zahanati na kwamba baadaye kutokana na ukubwa wa changamoto ya afya kwenye kata hiyo, mradi huo ulipandishwa hadi kuwa kituo cha afya.

Mtendaji wa Kata hiyo, Amiri Omar, akielezea ujenzi huo alisema unaendeshwa kwa nguvu za wananchi ikiwamo michango kwa kila mkazi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Masagalu, Ibrahim Kilama, ilieleza kuwa ujenzi huo ulianza mwaka 2017 kama zahanati, na utanufaisha wafanyakazi 747 utakapokamilika.

# Wanawake wapigania umiliki ardhi Ngorongoro watengwa

**Na Cynthia Mwilolezi, NGORONGORO**

WANAWAKE wanaopigania haki ya kumiliki ardhi katika maeneo mbalimbali Wilaya ya Ngorongoro Mkoa wa Arusha, wamekuwa wakitengwa na jamii kwa madai wanakiuka mila na desturi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, katika uchunguzi uliofanywa katika wilaya hiyo, kwa kushirikiana na Shirika la Hakiardhi, baadhi ya wananchi, viongozi wa serikali na mashirika ya kutetea haki za wanawake, walisema tatizo la wanawake kukosa haki ya kumiliki ardhi ni kubwa katika wilaya hiyo.

Mkurugenzi wa Shirika la Mimutie Women Organization (WMO),Rose Njilo, alisema hadi sasa wanawake kadhaa wamekuwa wakitengwa na jamii kutokana na kupambana kudai umiliki wa ardhi na kumtaja Taleng'o Ole Sayeti mmoja wa wanawake, aliyetengwa kutokana na kupinga kunyang'anywa ardhi.

"Hivi sasa kwenye sherehe amekuwa haalikwi na mambo mengi ashirikishwi inaonekana kama mkosaji baada ya kupinga kunyanyaswa na alipokonywa ardhi ambayo alirudishiwa baada ya kufikisha suala lake mahakamani na kupewa haki," alisema Njilo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Laretok -Le- Sheria na Haki za Binadamu Ngorongoro, (LASHEHABINGO), Charles Ndangoya, Mkazi wa Kijiji cha Wasso, Loliondo wilayani Ngorongoro, alisema ni muhimu jamii kutambua haki za wanawake kwani imekuwa ni changamoto kubwa na wamekuwa wakipokea malalamiko mengi ya migogoro ya umiliki wa ardhi, inayohusu wanawake, ambao wamekuwa wakidai haki hizo wakitengwa na kupigwa.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Rashid Taka, alisema mifumo dume katika jamii, mila na tamaduni za jamii za kifugaji ni changamoto kubwa, kuhusu haki z: wanawake katika wilaya hiyo, ali itaka jamii kubadilika na kutambua kila mtu ana haki ya kumilik mali halali katika jamii.

Taka alishauri kuwapo mida halo kuanzia ngazi za familia kujadili haki za wanawake na wanaume, kuandika wosia mapem: juu ya mgawanyo wa mali zao kwa kuwapa pia wanawake ili kupunguza migogoro isiyo ya lazim: katika jamii.